# MSAHAFU MTAKATIFU

# WA MUUNGU,

MWENYI AGANO LA KALE, NALO LILILO JIPYA,
YAMEFASIRIKA KATIKA LUGHA YA ZAMANI.

LONDON:
KIMEPIGWA CHAPA KWA
BRITISH AND FOREIGN BIBLE SOCIETY.
1895.

## MAJINA NA TARATIBU YA VITABU VYOTE VYA AGANO LA KALE.


| | SURA |
|---|---|
| Mwanzo | 50 |
| Kutoka | 40 |
| Mambo ya Walawi | 27 |
| Hesabu | 36 |
| Kumbukumbu ya Torati | 34 |
| Yoshua | 24 |
| Waamuzi | 21 |
| Ruth | 4 |
| 1 Samwil | 31 |
| 2 Samwil | 24 |
| 1 Wafalme | 22 |
| 2 Wafalme | 25 |
| 1 Mambo ya Siku | 29 |
| 2 Mambo ya Siku | 36 |
| Ezra | 10 |
| Nehemiya | 13 |
| Esther | 10 |
| Ayub | 42 |
| Zaburi | 150 |
| Methali | 31 |
| Koheleth ao Mhubiri | 12 |
| Uimbo wa Nyimbo | 8 |
| Isaya | 66 |
| Yeremiya | 52 |
| Maombolezo | 5 |
| Ezekieli | 48 |
| Danieli | 12 |
| Hosea | 14 |
| Yoel | 3 |
| Amos | 9 |
| Obadiya | 1 |
| Yunus | 4 |
| Mika | 7 |
| Nahum | 3 |
| Habakkuk | 3 |
| Zefaniya | 3 |
| Haggai | 2 |
| Zekariya | 14 |
| Malaki | 4 |


## MAJINA NA TARATIBU YA VITABU VYOTE VYA AGANO JIPYA.


| | SURA |
|---|---|
| Mattayo | 28 |
| Marko | 16 |
| Luka | 24 |
| Yohana | 21 |
| Matendo | 28 |
| Warumi | 16 |
| 1 Wakorintho | 16 |
| 2 Wakorintho | 13 |
| Wagalatia | 6 |
| Waefeso | 6 |
| Wafilipi | 4 |
| Wakolossai | 4 |
| 1 Wathessalonike | 5 |
| 2 Wathessalonike | 3 |
| 1 Timotheo | 6 |
| 2 Timotheo | 4 |
| Tito | 3 |
| Filemon | 1 |
| Waebrania | 13 |
| Yakobo | 5 |
| 1 Petro | 5 |
| 2 Petro | 3 |
| 1 Yohana | 5 |
| 2 Yohana | 1 |
| 3 Yohana | 1 |
| Yuda | 1 |
| Ufunuo | 22 |

# KITABU CHA KWANZA CHA MUSA,

# MWANZO.

**1** MWANZO aliziumba Muungu mbingu na
2 dunia. Dunia ikawa ukiwa utupu; ika-
wako giza juu ya uso wa kilindi: Roho ya
3 Muungu ikatulia juu ya uso wa maji. Mu-
ungu akanena, Uwe weupe; weupe ukawa.
4 Muungu akauona weupe, ya kuwa mwema;
Muungu akatenga kati ya weupe na giza.
5 Muungu akauita weupe Mchana, na giza
akaiita Usiku. Ikawa jioni ikawa assubuhi,
siku moja.
6 Akanena Muungu, Iwe nafasi kati ya
7 maji, ikayatenge maji na maji. Muungu
akaifanya nafasi, akayatenga maji yaliyo
chini ya nafasi na maji yaliyo juu ya nafasi:
8 ndivyo ilivyokuwa. Muungu akaiita nafasi
Mbingu. Ikawa jioni ikawa assubuhi, siku
ya pili.
9 Akanena Muungu, Yakusanyike maji ya-
liyo chini ya mbingu mahali pamoja, ikao-
nekane iliyo kavu: ndivyo ilivyokuwa.
10 Muungu akaiita iliyo kavu Inchi; na kusa-
nyiko la maji akaliita Bahari: Muungu
11 akaona ya kuwa mema. Akanena Muungu,
Inchi ichupuze uchupuko, mboga iotayo
mbegu, mti wa matunda uzaao matunda
kwa ginsi yake, mbegu zake ndani yake, juu
12 ya inchi: ndivyo ilivyokuwa. Inchi ikatoa
uchupuko, mboga iotayo mbegu kwa ginsi
yake, na mti uzaao matunda, mbegu zake
ndani yake kwa ginsi yake: Muungu aka-
13 ona ya kuwa mema. Ikawa jioni ikawa
assubuhi, siku ya tatu.
14 Akanena Muungu, Iwe mianga kwa na-
fasi ya mbingu, itenge mchana na usiku;
iwe kwa dalili, na kwa majira, na kwa siku
15 na miaka: nayo iwe kwa mianga kwa
nafasi ya mbingu iangaze juu ya dunia:
16 ndivyo ilivyokuwa. Muungu akaifanya
mianga mikubwa miwili; mwanga mkubwa
kuutawala mchana, na mwanga mdogo ku-
17 utawala usiku: nazo nyota. Muungu akai-
weka kwa nafasi ya mbingu, iangaze juu
18 ya dunia, ikatawale na mchana na usiku,
19 ikatenge weupe na giza: Muungu akaona
ya kuwa mema. Ikawa jioni ikawa assu-
buhi, siku ya 'nne.
20 Akanena Muungu, Kujawa yajawe maji
zilizo hayi, nazo zirukazo ziruke juu ya
21 inchi, usoni pa nafasi ya mbingu. Akawa-
umba Muungu nyamgumi wakubwa, na
zote zilizo hayi zitambaazo, yaliyojawa
nazo maji, kwa ginsi zao, na zote zirukazo
zenyi mabawa kwa ginsi zao: Muungu
22 akaona ya kuwa mema. Akawabariki Mu-
ungu, akinena, Mzidi, mkaongezeke, mka-
yajaze maji ya bahari, zikazidi zirukazo
23 inchini. Ikawa jioni ikawa assubuhi, siku
ya tano.
24 Akanena Muungu, Itoe inchi kilicho hayi
kwa ginsi yake, nyama, nazo zitambaazo,
nao walio hayi wa inchi kwa ginsi yake:
25 ndivyo ilivyokuwa. Akawafanya Muungu
walio hayi wa inchi kwa ginsi yake, na
nyama kwa ginsi yake, na killa kitambaacho
cha inchi kwa ginsi yake: Muungu akaona
26 ya kuwa mema. Akanena Muungu, Tum-
fanye Adamu kwa mfano wetu, mwenyi sura
yetu: wakamiliki juu ya samaki za bahari,
juu yao warukao mbinguni, juu ya nyama,
juu ya inchi pia, na juu yao wenyi kutambaa,
27 watambaao juu ya inchi. Muungu aka-
mumba Adamu kwa mfano wake yeye, kwa
mfano wa Muungu akamumba; mume na
28 mke akawaumba. Muungu akawabariki:
Muungu akawaambia, Mzidi, mkaongezeke,
mwijaze inchi, mkaitiishe; mkamiliki juu
ya samaki za bahari, juu yao warukao
mbinguni, na juu yao wote walio hayi
29 watambaao kwa inchi. Muungu akanena,
Bassi nimewapa mboga zote ziotazo mbegu
zilizopo usoni pa inchi yote, na killa mti
mwenyi tunda la mti uotao mbegu: kwenu
30 yatakuwa kwa chakula: na kwa killa nya-
ma ya inchi, na killa irukayo mbinguni, na
killa kitambaacho juu ya inchi, kilicho hayi,
majani yote ya mboga kwa chakula: ndivyo
31 ilivyokuwa. Muungu akaona killa alicho-
kifanya, nacho bassi chema sana. Ikawa
jioni ikawa assubuhi, siku ya sita.

**2** ZIKAMALIZIKA mbingu na dunia, na
2 jeshi lake pia. Siku ya saba Muungu aka-
maliza kazi yake aliyoifanya; akastarehe
siku ya saba katika kazi yake yote aliyoifa-
3 nya. Muungu akaibariki siku ya saba, aka-
itakasa; kwa sababu ndiyo aliyostarehe
katika kazi yake yote aliyoiumba Muungu,
akiifanya.
4 Hivi vizazi vya mbingu na dunia, ziki-
umbwa, siku alipozifanya BWANA Muungu
5 dunia na mbingu. Wala haujakuwako du-